*Tafsiri hii imefanywa na Social Development Direct na Translators without Borders kwa lengo la kufahamisha tu. Muungano wa Mashirika ya Uingereza yanayofanya kazi katika Maendeleo ya Kimataifa (BOND) hauwezi kuthibitisha usahihi wake.* Toleo rasmi la pekee lililoandikwa kwa Kiingereza linaweza kupatikana kwenye wavuti wa BOND *[*[Safeguarding policy templates | Bond](Safeguarding policy templates | Bond)*].'*

# Kulinda Usalama wa BOND
# Sera ya Kulinda Usalama

## Lengo

Lengo la sera hii ni kulinda watu, hasa watoto, watu wazima walio katika hatari na wanaofaidika kwa msaada, dhidi ya madhara yoyote yanayoweza kutokea kwa sababu kutangamana na [Shirika lisilo la Kiserikali]. Hii inajumuisha na madhara yanayotokana na:

- Mwenendo wa wafanyakazi au wafanyakazi wanaohusishwa na [Shirika lisilo la Kiserikali]
- Muundo na utekelezaji wa programu na shughuli za [Shirika lisilo la Kiserikali]

Sera hii inaweka wazi ahadi zilizotolewa na [Shirika lisilo la Kiserikali], na kuwaarifu wafanyakazi wake na wafanyakazi wanaohusishwa nao[1] kuhusu majukumu yao kuhusiana na kulinda usalama.

Sera hii haielezei:

- Unyanyasaji wa kijinsia mahali pa kazi - hii inaelezewa chini ya Sera ya Kupambana na Uonevu na Unyanyasaji wa [Shirika lisilo la Kiserikali][2]
- Kero za kulinda usalama katika jamii pana zisizotekelezwa na [Shirika lisilo la Kiserikali] au wafanyakazi wanaohusishwa

## Kulinda usalama ni nini?

Nchini Uingereza, kulinda usalama kunamaanisha kulinda afya za watu, ustawi na haki za binadamu, na kuwawezesha kuishi bila madhara, dhuluma na kutelekezwa[3]

Katika sekta yetu, tunaelewa kuwa inamaanisha kulinda watu, wakiwemo watoto na watu wazima walio katika hatari, dhidi ya madhara yanayotokana na kutangamana na wafanyakazi wetu au programu.

Ufafanuzi zaidi unaohusiana na kulinda usalama umetolewa katika sherehe hapa chini.

## Upeo

- Wafanyakazi wote waliopewa kandarasi na [Shirika lisilo la Kiserikali]

[1] Tazama 'Upeo' kwa ufafanuzi wa wafanyakazi wanaohusishwa
[2] Baadhi ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali sasa zinajumuisha uonevu na unyanyasaji mahali pa kazi katika nyenzo zao za kulinda usalama, kwa kuwa inahusiana na madhara yanayosababishwa na kutangamana na wafanyakazi na programu zetu. Hata hivyo taratibu zinazoambatana za kushughulikia uonevu na unyanyasaji mahali pa kazi huenda zikawa tofauti, kwa sababu ya tofauti za kisheria katika kushughulikia matukio ya mahali pa kazi
[3] NHS (United Kingdom National Health Service) 'Kulinda Usalama ni nini? Rahisi Kusoma' 2011

- Wafanyakazi wanaohusishwa wakati wa kufanya kazi au ziara zinazohusiana na [Shirika lisilo la Kiserikali], ikijumuisha sio tu wafuatao: washauri; wafanyakazi wa kujitolea; wanakandarasi; wageni wa programu wakiwemo waandishi wa habari, watu mashuhuri na wanasiasa

# Taarifa ya Sera

[Shirika lisilo la Kiserikali] inaamini kuwa kila mtu tunayetangamana naye, bila kujali umri, utambulisho wa jinsia, ulemavu, mwelekeo wa kijinsia au asili ya kabila ana haki ya kulindwa dhidi ya aina zote za madhara, dhuluma, kutelekezwa na unyonyaji. [Shirika lisilo la Kiserikali] halitaruhusu dhuluma na unyanyasaji unaofanywa na wafanyakazi wake au wafanyakazi wanaohusishwa.

Sera hii itashughulikia mada zifuatazo za kulinda usalama [kama inavyofaa]: kulinda watoto, kulinda usalama wa watu wazima, na kinga dhidi ya unyonyaji wa kijinsia na dhuluma. Mada hizi muhimu za kulinda usalama zinaweza kuwa na sera na taratibu tofauti zinazohusiana nazo (tazama Sera zingine zinazofaa).

[Shirika lisilo la Kiserikali] linajitolea kushughulikia kulinda usalama wakati wote wa kazi yao, kupitia nguzo tatu za kuzuia, kupiga kuripoti na kutoa majibu.

# Kuzuia

## Majukumu ya [Shirika lisilo la Kiserikali]

[Shirika lisilo la Kiserikali]:

- Litahakikisha kuwa wafanyakazi wote wanapata, wanafahamu, na wanajua majukumu yao kwenye sera hii
- Litabuni na kutekeleza programu na shughuli zake zote kwa njia ambayo inalinda watu dhidi ya hatari yoyote ya madhara yanayoweza kutokea kutokana na kutangamana na [Shirika lisilo la Kiserikali]. Hii inajumuisha njia ambayo habari kuhusu watu binafsi katika programu zetu hukusanywa na kujadiliwa
- Litatekeleza taratibu kali za kulinda usalama wakati wa kuajiri, kusimamia na kuwaweka kazini wafanyakazi wake na wafanyakazi wanaohusishwa
- Litahakikisha wafanyakazi wanapata mafunzo kuhusu kulinda usalama katika ngazi inayolingana na wajibu wao katika shirika
- Litafuatilia ripoti za kero za kulinda usalama mara moja na kulingana na utaratibu unaofaa

## Majukumu ya wafanyakazi

**Kulinda Usalama wa Watoto**

Wafanyakazi wa [Shirika lisilo la Kiserikali] na wafanyakazi wanaohusishwa hawapaswi:

- Kushiriki katika matendo ya ngono na mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka 18
- Kuwanyonya au kuwadhulumu kijinsia watoto
- Kumdhulumu mtoto kimwili, kihisia au kumnyanyasa kisaikolojia, au kutelekeza

- Kushiriki katika shughuli zozote za kibiashara za unyonyaji na watoto ikiwemo ajira ya watoto au usafirishaji haramu

**Kulinda Usalama wa watu wazima**

Wafanyakazi wa [Shirika lisilo la Kiserikali] na wafanyakazi wanaohusishwa hawapaswi:

- Kuwadhulumu kijinsia au kuwanyonya watu wazima walio katika hatari
- Kumdhulumu mtu mzima aliye katika hali hatari kimwili, kihisia au kumnyanyasa kisaikolojia, au kumtelekeza

**Ulinzi dhidi ya unyonyaji wa kijinsia na dhuluma**

Wafanyakazi wa [Shirika lisilo la Kiserikali] na wafanyakazi wanaohusishwa hawapaswi:

- Kubadilisha pesa, ajira, bidhaa au huduma kwa ajili ya tendo la ngono. Hii inajumuisha na ubadilishaji wowote wa msaada unaokusudiwa wanaofaidika kwa msaada
- Kushiriki katika mahusiano ya kingono na wanaofaidika kwa huduma kwa kuwa mahusiano hayo kimsingi yanahusisha mamlaka yasiyotoshana

Kwa kuongezea, wafanyakazi na wafanyakazi wanaohusishwa na [Shirika lisilo la Kiserikali] wanalazimika:

- Kuchangia katika kuunda na kudumisha mazingira ambayo yanazuia ukiukaji wa kulinda usalama na kuendeleza utekelezaji wa Sera ya Kulinda Usalama
- Kupiga ripoti kuhusu kero zozote au tuhuma za ukiukaji wa kulinda usalama na mfanyakazi au wafanyakazi wanaohusishwa na [Shirika lisilo la Kiserikali] kwa mfanyakazi husika

# Kuwezesha upigaji wa ripoti

[Shirika lisilo la Kiserikali] litahakikisha kuwa njia salama, zinazofaa, na zinazopatikana za kupiga kuripoti kuhusu kero za kulinda usalama zipo kwa wafanyakazi na jamii tunayofanya kazi nayo.

Mfanyakazi yeyote anayepiga ripoti kuhusu kero au malalamishi kupitia njia rasmi za kufichua uhalifu (au wakiomba) watalindwa na Sera ya Kifichua Matendo yasiyofaa Mahali pa Kazi (Kufichua Uhalifu) ya [Shirika lisilo la Kiserikali].

[Shirika lisilo la Kiserikali] pia litakubali malalamishi kutoka kwa vyanzo vya nje kama vile wanajamii, washirika na asasi rasmi.

### Jinsi ya kupiga kuripoti ya kero ya kulinda usalama

Wafanyakazi ambao wana malalamishi au kero zinazohusiana na kulinda usalama wanapaswa kupiga kuripoti mara moja kwa Mratibu wa Kulinda Usalama [inavyofaa] au msimamizi mhusika. Ikiwa mfanyakazi hahisi vizuri kupiga kuripoti kwa Mratibu wa Kulinda Usalama au Msimamizi wake (kwa mfano ikiwa wanahisi kuwa ripoti hiyo haitachukuliwa kwa uzito, au ikiwa msimamizi huyo anahusika na kero hiyo) wanaweza kupiga kuripoti kwa mfanyakazi mwingine yeyote anayefaa. Kwa mfano, huyu anaweza kuwa msimamizi mkuu au mmoja wa Timu ya Rasilimali Watu.

[Toa maelezo ya mawasiliano]

# Jibu

[Shirika lisilo la Kiserikali] litafuatilia ripoti na kero za kulinda usalama kulingana na sera na utaratibu, na wajibu wa kisheria (tazama Taratibu za kupiga kuripoti na kushughulikia kero za kulinda usalama katika Sera zingine zinazofaa).

[Shirika lisilo la Kiserikali] itatumia hatua zinazofaa za kinidhamu kwa wafanyakazi watakaopatikana wakikiuka sera.

[Shirika lisilo la Kiserikali] litatoa msaada kwa manusura wa madhara yanayosababishwa na wafanyakazi wake au wafanyakazi wanaohusika, bila kujali ikiwa majibu rasmi ya ndani yametekelezwa (kama vile uchunguzi wa ndani). Maamuzi kuhusu usaidizi yataongozwa mnusura mwenyewe.

# Usiri

Ni muhimu kwamba usiri udumishwe katika hatua zote za mchakato wakati wa kushughulikia kero za kulinda usalama. Habari inayohusiana na kero na usimamizi wa kesi unapaswa kushirikiwa kwa hitaji la kujua kiini tu, na inapaswa kuwekwa kisalama kila wakati.

### Sera zingine zinazofaa

Kanuni ya Maadili

Sera ya Kupinga Uonevu na Unyanyasaji

Sera ya Kufichua (Kufichua uhalifu) Matendo yasiyofaa Mahali pa Kazi

Sera ya Kulinda Usalama wa watoto

Sera ya Kulinda Usalama wa watu wazima

Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono (PSEA)

Sera ya Malalamishi

Taratibu za kupiga ripoti na kushughulikia kero za kulinda usalama

Taratibu za kulinda usalama katika uajiri wa wafanyakazi

Sera zingine kama inavyofaa

# Sherehe ya Masharti

**Wanaofaidika kwa Msaada**

Mtu ambaye anapokea bidhaa au huduma moja kwa moja kutoka kwa programu ya [Shirika lisilo la Kiserikali]. Kumbuka kuwa utumizi mbaya wa mamlaka pia unaweza kutumika kwa jamii pana ambayo Shirika lisilo la Kiserikali linahudumia, na pia inaweza kujumuisha unyonyaji kwa kutoa mtazamo wa kuwa katika nafasi ya mamlaka.

**Mtoto**

Mtu aliye chini ya umri wa miaka 18

**Madhara**

Ukiukwaji wa kisaikolojia, kimwili na ukiukwaji mwingine wowote wa haki za mtu binafsi

**Madhara ya kisaikolojia**

Dhuluma ya kihisia au kisaikolojia, ikijumuisha (sio tu) kuhujumiwa na kudunishwa kama vile kuitwa jina baya, kukosolewa kila wakati, kudharauliwa, kuaibishwa kila mara, kufungwa pweke na kutengwa

**Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma na Unyanyasaji wa Kingono (PSEA)**

Neno linalotumiwa na jamii ya msaada wa kibinadamu na maendeleo kumaanisha kuzuia unyonyaji wa kijinsia na dhuluma ya watu walioathiriwa na wafanyakazi au wafanyakazi wanaohusika. Neno hili linatokana na Taarifa rasmi ya habari (Bulletin) ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa juu ya Hatua Maalumu za Ulinzi dhidi ya Unyonyaji wa Kijinsia na Dhuluma (ST / SGB / 2003/13)

**Kulinda usalama**

Nchini Uingereza, kulinda usalama kunamaanisha kulinda afya za watu, ustawi na haki za binadamu, na kuwawezesha kuishi bila madhara, dhuluma na kutelekezwa[4]

Katika sekta yetu, tunaelewa kuwa inamaanisha kulinda watu, wakiwemo watoto na watu wazima walio katika hatari, dhidi ya madhara yanayotokana na kutangamana na wafanyakazi wetu au programu. Ufafanuzi wa mmoja wa wafadhili ni kama ifuatavyo:

Kulinda usalama kunamaanisha kuchukua hatua zote za busara kuzuia madhara, hasa unyonyaji wa kijinsia, dhuluma na unyanyasaji wa kijinsia kutokea; kulinda watu, hasa watu wazima na watoto walio katika hali hatarishi, dhidi ya madhara hayo; na kukabiliana ipasavyo na madhara yanapotokea.

Ufafanuzi huu unatokana na maadili na kanuni zetu na kuunda desturi zetu. Unaweka makini zaidi katika kuzuia na kushughulikia madhara kutoka kwa uwezekano wowote, halisi au jaribio la matumizi mabaya ya mamlaka, uaminifu, au udhaifu, hasa kwa madhumuni ya kingono.

Kulinda usalama kunatumika kila wakati na bila ubaguzi katika programu zetu zote, washirika na wafanyakazi. Kunahitaji kutambua kimbele, kuzuia na kulinda dhidi ya hatari zote za madhara, unyonyaji na dhuluma na kuwa na mifumo iliyokomaa, ya uwajibikaji na uwazi ya kukabiliana, kupiga ripoti na kujifunza hatari zinapotokea. Mifumo hiyo lazima iwe na msingi wake kwenye mnusura na iwalinde washukiwa hadi wathibitishwe kuwa na hatia.

Kulinda usalama kunaweka wanaofaidika kwa msaada na watu walioathirika katika kiini cha yote tunayoyafanya.

**Dhuluma ya kijinsia**

Neno 'dhuluma ya kijinsia' linamaanisha hali halisi kuingiliwa au kutishiwa kingono, iwe kwa nguvu au chini ya hali zisizo sawa au za kulazimisha.

**Unyonyaji wa kijinsia**

Neno 'unyonyaji wa kijinsia' linamaanisha jaribio au unyanyasaji halisi katika hali hatarishi, mamlaka yasiyotoshana, au uaminifu, kwa madhumuni ya kingono, ikijumuisha, sio tu, kufaidika kifedha, kijamii au kisiasa kutokana na unyonyaji wa kingono wa mtu mwingine. Ufafanuzi huu unajumuisha usafirishaji haramu wa binadamu na utumwa wa kisasa.

**Mnusura**

Mtu ambaye amedhulumiwa au kunyonywa. Neno 'mnusura' hutumiwa mara nyingi kwa kupendelewa kuliko 'mwathiriwa' kwani linachukuliwa kumaanisha nguvu, uthabiti na uwezo wa kunusurika, hata hivyo ni chaguo la mtu binafsi jinsi anavyotaka kujitambulisha.

**Mtu mzima aliye katika hatari**

Wakati mwingine pia linarejelea mtu mzima aliye katika hali hatarishi. Mtu ambaye anahitaji au anaweza kuhitaji utunzaji kwa sababu ya ulemavu wa akili au nyingine, umri au maradhi; na ambaye huenda asiweze kujitunza mwenyewe, au asiyeweza kujilinda dhidi ya madhara makubwa au unyonyaji.

[4] NHS (United Kingdom National Health Service) 'Kulinda Usalama ni nini? Rahisi Kusoma' 2011